

## DIRA YA GABRIELLA

Gabriella ni shirika lisilo la kiserikalil lililozanzishwa mnamo july 2009 kwa ajili ya kuhakikisha watoto na vijana wenyewe uhitaji maalum wanatambulika mapema, wanachunguzwa na kupatiwa fursa stahiki kwa ajili ya kuweza kukubalika na kuthaminika katika jamii kama mmoja wa wanajamii

Kituo kina shule ya awali ambayo ni jumishi, darasa maalumu kwa wenyewe uhitaji maalum (special need class), kujifunza ujuzi mbalil mbali . wataalum wetu wanalenga kuwasaidia pia watoto wenyewe usonji na matatizo katika kujifunza wawewe kujitegemea ikiwa ni pamoja na kuelimisha jamii mahitaji na uwezo wa watoto na vijana hawa



Kwa habari Zaidi wasiliana  
na mkurugenzi  
Brenda Shuma  
[gabriellacentre@hotmail.com](mailto:gabriellacentre@hotmail.com)

0713456727  
0766559968

Gabriella Children's  
Rehabilitation Centre

P.O. Box 9626  
Sambarai Kibosho Road  
Moshi, Kilimanjaro, Tanzania

<http://www.gabriellarehab.org>

**Gabriella**  
Rehab Centre

Gabriella Children's  
Rehabilitation Centre



**HUDUMA YA  
UTENGEMAO**

kuboresha thamani ya maisha ya  
kila siku ya mtoto na familia

# Good, Better, Best, Gabriella!

Teresia ni kijana aliyefika kituoni miaka miwili iliyopita na ilikuwa ni baada ya kukataa tama kutokana na kuwepo shulenii kwa miaka mingi bila kuweza kusoma na kuandika. Alipofika kituoni watalum wetu waligundua kuwa hawezi kujifunza kwa mfumo uliokuwa unatumika shulenii kutoka na kuwa ana uhitaji maalum katika namna ya kujifunza (anajifunza polepole)

Alipatiwa fursa mbalimbali kituoni na hatimaye akaonyesha anapenda mapishi zaidi. Sasa ameweza kupika karanga na bisi(popcon) na sasa anajitegemea nyumbani kwao na anasaidia mahitaji ya familii



## Huduma zitolewazo kituoni

### WIKI MAALUM YA MAZOEZI

Huduma hii inalenga watoto wenyewe ulemavu wa akili na viungo kuanzia umri wa o hadi miaka 14 kwa kuwapatia fursa ya kumwona daktari bingwa wa watoto na kupata fursa ya mazoezi kutoka watalum wetu. Ikitegemea hali ya mtoto mazoezi hutolewa kwa mfululizo au kwa kupishana. Pia mzazi au mlezi anapata fursa ya kujumuika na wanzake na pia anapatiwa fursa ya kujifunza namna ya kuendelea na mazoezi nyumbani  
HUDUMA YA AWALI (MONTESSORI KINDAGATEN )

Hii inaendeshwa siku za kazi kuanzia jumatatu mpaka ijumlaha. Tunatoa huduma hii kwa watoto wenyewe uhitaji maaluma na wale wasiokuwa na uhitaji maalum. Mfumo wa Montessori hutumika kumsaidia mtoto kujifunza kwa kutumia milango yake Yote ya fahamu. Inayofanya kujifunza kuwe rahisi na yenye kufurahiwa

Watoto wanapata huduma ya kukaa mpaka saa tisa jioni iwapo mzazi anauhitaji huo.

### UCHUNGUZI NA USHAURI

Watoto wenyewe umri wa shule na walioko mashulenii wanapata fursa ya kufanyiwa uchunguzi wa kina na mahtaji yao kujulikana na kushughulikiwa mapema iwezekanavyo. Kituo kinafanya kazi kwa kushirikiana na shule za msingi na vitengo maalumu vilivyopo katika shule za misingi katika kanda ya kaskazini. Pia watoto wanapata fursa ya mjumuisho na watalamu wetu kuwafuatiulia kwa karibu na kushauriana na waalimu.pamoja na fursa ya kuonwa na daktari bingwa wa watoto anaye kuja kuona watoto wenyewe uhitaji wa ushauri wake .

### KUJIFUNZA UJUZI (SKILLS TRAINING)

Huduma hii ni kwa wale watoto wenyewe ulemavu wa akili Hii inalenga kuwafundisha watoto ujuzi mbali mbali wa kazi za mikono, shughuli za kila siku, namna ya kufanya mauzo ya vitu na utambuzi wa pesa n.k watalam wetu wanatumia mbinu mbalimbali kuweza kufikia malengo hayo

### Kazi za nje ya kituo na kutembelea majumbani

Watalum na waalimu kituoni hutembelea nje ya kituo kwa nia ya kuelimisha iamii na kuwawezesha